**HOTUBA YA MHESHIMIWA *BALOZI* MAHAMOUD THABIT KOMBO, WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI KATIKA MKUTANO MKUU MAALUM WA TANZANIA CHEMBER OF COMMERCE, INDUSTRIES & AGRICULTURE (TCCIA) TAIFA UTAKAOFANYIKA KATIKA HOTELI YA TIFFANY DIAMOND – DAR ES SALAAM TAREHE 22 OKTOBA 2025**

- **Bw. Vicent Minja, rais wa TCCIA,**
- **Dkt. Godwil Wanga, Katibu Mtendaji wa Baraza la Biashara la Taifa,**
- **Wajumbe wa Bodi ya TCCIA,**
- **Viongozi wastaafu wakiongozwa na Mzee David Mwaibula,**
- **Wenyeviti wa TCCIA kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara,**
- **Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa,**
- **Watendaji wa TCCIA Taifa na Mikoa, wakiongozwa na Bw. Oscar Kissanga, Mkurugenzi Mtendaji,**
- **Wageni Waalikwa,**
- **Mabibi na Mabwana,**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Kazi Iendelee…***

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,**

Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa fursa hii adhimu ya kukutana nanyi. Pili, ninashukuru uongozi wa TCCIA kwa kunialika kuungana nanyi katika mkutano huu muhimu wa Taasisi yenu.

Kwa miaka mingi, nimeona TCCIA ikipitia changamoto ikiwemo changamoto za kiutawala, za ushirikishaji makundi yote, za ushirikiano na Serikali. Lakini zaidi ya hayo, nimeona TCCIA ikipoteza fursa kubwa.

TCCIA imekuwa ikipoteza fursa ya kuwa injini halisi ya Diplomasia ya Uchumi ya Tanzania. Fursa ya kufungua milango katika masoko ya kimataifa. Fursa ya kuwa daraja kati ya biashara za Kitanzania na fursa za duniani.

Leo ninaongea nanyi siyo tu kama Waziri - bali kama rafiki anayetaka kuona TCCIA ikijikita katika kuhakikisha inatumi uwezo wake kamili kama

chombo muhimu katika kufanikisha diplomasia ya Uchumi katika Taifa letu.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,**

Nichukue fursa hii kuwasimulia uzoefu wangu nilipokuwa Balozi wa Tanzania nchini Italia ambapo niliamua kufanya kazi tofauti ili kuweza kufikia malengo ya Ubalozi. Sikukaa ofisini kusubiri diplomasia ya kawaida. Niliamua kuanzisha Jukwaa la biashara kati ya Tanzania na Italia (Tanzania – Italy Business Forum) jukwaa ambalo linaunganisha wafanyabiashara, viongozi wa sekta binafsi, na Serikali ya Tanzania na Italia. **Na hapa naomba kuwapa matokeo ya Jukwaa hilo.**

Mwaka huu tu, tulifanikisha mkutano wa nne wa jukwaa hilo. Tumeshuhudia mambo yafuatayo;

I. Kusainiwa kwa Mikataba ya uwekezaji ya zaidi ya dola milioni 150;
II. Wafanyabiashara wa Kitanzania wakifungua biashara za moja kwa moja Italia;
III. Kampuni za Kiitaliano zikiwekeza kwenye kilimo, viwanda, na utalii Tanzania na;
IV. Fursa za kupata nafasi za mafunzo na teknolojia kwa vijana wetu katika vyuo mbalimbali nchini Italia.

Haya yote yalitokea kwa sababu moja: Tuliunganisha nguvu za sekta binafsi na Serikali, Aidha, tulitoka kuwatafuta wawekezaji na sio kuwasubiri kuja Ofisini.

***Swali langu kwenu leo: Kama tulifanya hivyo Italia - Nchi moja - je, TCCIA haiwezi kufanya zaidi Duniani?***

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,**

Diplomasia ya Uchumi si kazi ya Serikali peke yake. Niwaambie ukweli kuwa, Diplomasia ya uchumi haiwezi kufanikiwa bila sekta binafsi.

Serikali inaweza kusaini mikataba ya Biashara na ninyie wafanyabiashara mnaotekeleza mikataba hiyo. Serikali inaweza kuanzisha ushirikiano ni TCCIA na sekta binafsi wanaofanya ushirikiano kuwa tija kwa Taifa letu. Hii ndiyo siri ya nchi zinazofanikiwa duniani.

Nchi kama Korea Kusini - Korean Chamber of Commerce & Industry ni mshirika moja kwa moja wa serikali katika kudhibiti uwekezaji wa nje na biashara za kimataifa.

Nchi kama Singapore - *Singapore Business Federation* inasimamia diplomasia ya biashara kwa ushirikiano na vyombo vya Serikali.

Nchi kama Rwanda - *Private Sector Federation* ni sehemu ya kikosi cha Taifa kinachosafiri kimataifa kutafuta masoko.

***Swali langu kwenu Tanzania tunasubiri nini?***

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,**

Leo nawapongeza kwa kuboresha Katiba yenu. Lakini ninawashauri mboreshe zaidi - mboreshe Dira yenu.

**Ni vema TCCIA iwe:**

### i. MSHAURI MKUU WA SERIKALI KATIKA BIASHARA YA KIMATAIFA

Hamna sera ya biashara ya kimataifa inapaswa kupitishwa bila TCCIA kuchangia. Hamna mikataba ya kibiashara inapaswa kusainiwa bila mchango wa sekta binafsi.

### ii. KUONGOZA MAKUNDI YA WAFANYABIASHARA KIMATAIFA

TCCIA inapaswa kubuni na  kuongoza safari za wafanyabiashara kwenda Nchi mbalimbali. Na sio tu kusubiria Serikali kuambatana nao bali TCCIA kutafuta fursa na kuanzisha mashirikiano nje ya Nchi na kuandaa safari zenu binafsi.

### 3. DARAJA KWA WAWEKEZAJI WA KIGENI

Kila mwekezaji anayetaka kuja Tanzania anapaswa pia kupata uzoefu kutoka TCCIA. Kila biashara ya Kitanzania inayotaka kwenda nje anapaswa kupata msaada wa taarifa muhimu kutoka TCCIA.

### 4. MWANASHERIA WA WAFANYABIASHARA WA KITANZANIA

Wafanyabiashara wetu wanapofikwa na changamoto katika masoko ya nje, TCCIA lazima iwe tayari kushirikiana na mabalozi wetu kutatua matatizo.

### 5. MFUMO WA HABARI ZA MASOKO

TCCIA lazima iwe na mfumo maalum wa kuwa na taarifa za awali kuhusu fursa za biashara, mabadiliko ya sera, na fursa za uwekezaji duniani kote.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,**

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina Mabalozi, Wakuu wa Misheni na Konseli Kuu katika Nchi zaidi ya 45 na miji ya kibiashara mitano duniani kila mmoja wao ni kitovu cha fursa.

**Leo hii naahidi:**

- Kila Balozi wangu atakuwa na jukumu la kuhuisha ushirikiano na TCCIA;
- Nawaahidi Wizara itakuwa inaandaa *Economic Diplomacy Forum* kati ya Wizara na TCCIA;
- Tutaunganisha TCCIA na *Business Forums* za Nchi ambazo tunashirikiana nazo;
- Tuko tayari kusaidia TCCIA kufungua ofisi za uwakilishi katika vitovu vya kiuchumi duniani kama vile Dubai, Beijing, lakini hili litahitaji pia utayari wa TCCIA.

## Changamoto Nilizoziona - Na Suluhisho

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,**

Ninajua baadhi ya changamoto ambazo TCCIA inazo ni pamoja na:

- Ushirikiano dhaifu kati ya Taifa na Mikoa;
- Uwakilishi mdogo wa wanawake na vijana;
- Changamoto za rasilimali fedha kwa ajili ya uendeshaji; na
- Kukosekana kwa teknolojia.

Lakini changamoto hizi zote zinaweza kushughulikiwa ikiwa tutaunganisha nguvu kwa pamoja:

i. Serikali itasaidia kutafuta mafunzo, teknolojia, na ushirikiano wa kimataifa;
ii. Wadau wa kimataifa watasaidia kupitia uwekezaji na ushirikiano.

TCCIA lazima iwe taasisi inayoaminiwa na wafanyabiashara, na serikali, na wadau wa maendeleo kwa ujumla.

## Matarajio ya Wizara yangu.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,**

Ninatarajia kuona TCCIA ikisimama imara katika mazungumzo ya kimataifa. Ninatarajia kuona TCCIA ikiongoza safari za wafanyabiashara walau mara mbili kwa mwaka. Ninatarajia kuona TCCIA ikishirikiana na vyombo vya nje kama *African Business Forum, COMESA Business Council, na International Chamber of Commerce*. Ninatarajia kuona TCCIA ikiwa na mfumo mzuri wa habari utakao taarifu umma na wafanyabiashara kwa ujumla. **Haya si ndoto ni mambo yanayofanyika kila siku katika nchi nyingine. Kwa nini isiwe Tanzania?**

***Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,***

Napenda kumalizia kwa kusema kuwa, Tanzania safari ya kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050. Tanzania inaelekea kuwa nchi ya uchumi wa kati wa juu (high middle-income country) ifikapo 2050. Ili kufikia huko tunahitaji kuwa na sekta binafsi yenye nguvu na imara.Hatufikii huko bila diplomasia ya uchumi inayoshirikiana na sekta binafsi.

**Ndugu Wajumbe wa Mkutano Mkuu,**

Leo hii mko kwenye hatua muhimu kuboresha Katiba yenu. Mimi, kama Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, niko tayari kushirikiana nanyi kuhakikisha Taifa letu linafikia malengo yetu ya maendeleo kupitia mchango mkubwa wa Sekta Binafsi.

Kabla sijamaliza, nawapeni changamoto moja:

Mwaka ujao muda kama huu, nitapenda kusikia TCCIA imefungua Ofisi Dubai, kutafuta masoko China, na India, namna mlivyo unganisha nguvu na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kufungua milango ya mashirikiano.

**KWA HESHIMA, SASA NINAFUNGUA RASMI MKUTANO MKUU MAALUM WA TCCIA TAIFA.**

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Kazi Iendelee!***

**Asanteni sana.**